*AAP* 51 (1997): 83-94

# "HAMMATBIHI WAHAMMABIHA": FASIHI YA KISWAHILI NA KISA CHA YUSUF.

RIDDER H. SAMSOM

The story of Joseph (in the Bible), Yusuf (in the Quran), has inspired literatures in many languages. This paper explores how some Swahili writers and translators have dealt with this inspiration, the implications for their language use and the way they have interpreted Yusuf as a theme for their writings. After a brief introduction on the importance of the story itself and putting the focus on a major theme of the plot, the following works are discussed: the new Quran translation by Sh Ali Muhsin (1995), a short novel by Mzee Salim A. Kibao (1975), two short stories by Amur bin Nasur il-Omeiri (1894), the utenzi *Qissat-il Yusuf* (1913) and Abdulrazak Gurnah's English written novel *Paradise* (1995). The paper concludes with the observation that in analyzing how these Swahili writers have integrated the story of Yusuf in their writings, prose as well as poetry, it becomes clear that attempts in defining what is 'foreign' (or 'Oriental') and what is 'indigenous' (or 'African') are bound to fail

## Utangulizi

Huko Afrika Magharibi Wafulbe huandikiwa kombe lenye maneno hayo 'Hammatbihi wa Hammabiha' wanapotaka wapendwe na mtu wanayempenda. Maneno hayo huandikwa kwenye kibao yakakoshwa kwa maji kisha maji hayo yakanywewa ili Mungu ampe yule mtu msaada kumpatia atakayo.[1]

Msichana wa Kiswahili anapomuuliza bibi yake kwa sababu gani anayo mistari kwenye vitanga vya mikono yake, huambiwa kuwa wanawake walikuwa wanajikata mikono yao wakati Sayidna Yusuf alipopita mbele yao maana alikuwa ni mzuri sana.

Naye mvulana wa Kiswahili kila Alkhamis anyolewapo kisogo chake na kutotaka na kufanya fujo, huambiwa asikatae, maana atakuwa mzuri na kupendeza kama Yusuf.[2]

Kwa hakika si katika ustaarabu wa Kiswahili tu ambapo Nabii Yusuf amepewa hadhi kwa kiasi kikubwa mpaka ameingia katika mila ya watu na misemo ya kila siku. Hadithi yake hujulikana sana kutoka Biblia na Quran, kwa Mayahudi na Wakristo na Waislamu. Tena si ajabu kwamba hadithi hii imewavutia watu sana kwa sababu ya maudhui yake: muna tabia nyingi za binadamu ambazo tunaziona muhimu - mapenzi na chuki, uaminifu na uhaini, rehema na kisasi, kumfadhili mtu na kumkhini, wema na uovu.

---

[1] Namshukuru Dk Aliou Mohamadou wa INALCO (Paris) aliyenieleza hayo tulipokutana huko Leipzig, Aprili 3-5, 1997

[2] Vile vile shukrani zangu zimwendee Malim Yahya Ali Omar wa Mambasa kwa maelezo hayo, London, SOAS, Aprili 16, 1997

Pia Qurani yenyewe inatamka mwanzo wa sura hii kuwa (na yafuatayo ni tafsiri kwa Kiswahili ya Sh Abdallah Farsy: 1969): *"Sisi tunakusimulia simulizi nzuri kwa kukufunulia Qurani hii"* au, katika tafsiri yake kwa Kiingereza ya Sh Abdallah Yusuf Ali (1989:546)

> We do relate unto thee
> The most beautiful of stories,
> In that We reveal to thee
> This (portion of the) Quran:

Naye Sh Abdallah Yusuf Ali anaeleza katika maelezo yake pembeni (1989:546, Note 1631):

> **Most beautiful of stories:** see Introduction to this Surah. Eloquence consists in conveying by a word or hint many meanings for those who can understand and wish to learn wisdom. Not only is Joseph story "beautiful" in that sense; Joseph himself was renowned for manly beauty: the women of Egypt, called him a noble angel (12:31), and the beauty of his exterior form was a symbol of the beauty of his soul

Basi madhumuni ya makala haya ni kutazama vipi maudhui ya kisa chaYusuf yalivyotumiwa na waandishi mbalimbali katika tungo za namna mbalimbali katika fasihi ya Kiswahili."

**Qissat-al Yusuf: kisa chenyewe**

Kiini cha habari ya 'Yusufu mwanawe Yakobo' katika Biblia na 'Yusuf bin Yaaqubu' katika Qurani hakina tafauti kubwa baina ya mapokeo hayo mawili. Kwa vile mifano ya fasihi ya Kiswahili nitakayotoa katika makala haya imeathiriwa na Qurani, nimetumia tafsiri mbali mbali za Qurani kwa Kiswahili (taz. 'Marejeo').

Qurani inaeleza habari ya Yusuf katika aya 111 za Surat-alYusuf. Ndoto ya Yusuf ambayo baba yake alimwonya asiwasimulie nduguze *"wasije wakakufanyia vitimbi"* imesimuliwa katika aya 4 - 6. Vitimbi vya kaka zake walivyomfanyia Yusuf vimeelezwa kutoka aya 23 - 29. Baada ya kupelekwa Misri na kuuzwa akawa mtumwa na kutamaniwa na mkewe "'Aziz" ambaye hilo neno "'Aziz" limetafisiriwa kwa 'waziri' (Sh Abdallah) au 'Mheshimiwa' (Sh. Ali) au 'diwani' (Godfrey Dale):

> Na yule bibi wa nyumba aliyo kuwamo Yusuf alimtamani kinyume cha nafsi yake, na akafunga milango. Akamwambia: Njoo! Yusuf akasema: Audhubillahi! Najikinga na Mwenyezi Mungu. Huyu bwana wangu kaniweka maskani nzuri, na hakika wenye kudhulumu hawatengenekewi. Na hakika yule mwanamke alimtamani, na Yusuf angeli mtamani lau kuwa hakuona ishara ya Mola wake Mlezi.

Hayo yote yameelezwa katika aya 23-29. Kwa kuthibisha kuwa yeye *"hayumo katika upotovu ulio dhaahiri"* (aya 30), ingawa kabla (28) shahidi alikuwa ameonyesha kanzu yake imechanwa kwa nyuma, mkewe 'Aziz akampitisha Yusuf mbele ya *"wanawake wa mjini"* nao *"wakajikata mikono yao. Wakasema: Hasha Lillahi! Huyu si mwaanadamu. Hakuwa huyu ila ni Malaika mtukufu."* (31). Basi Yusuf akatiwa kifungoni (35), akawaagulia wafungwa wenzake wawili ndoto zao (36-42) na kisha kumwagulia mfalme mwenyewe ndoto zake (45-49) na *"Basi namna hivi tukampa Yusuf cheo katika nchi hii"* (56). *"Mke wa Mheshimiwa akasema: Sasa haki imedhihiri. Mimi ndiye niliye mtaka kinyume na nafsi yake, na hakika yeye ni katika wa kweli"* (51). Ndugu zake wakafunzwa na ndoto yake ikawa ni kweli: *"Na walipo ingia kwa*

*Yusuf aliwakumbatia wazazi wake na akasema: Ingieni Misri, Inshallah, mmo katika amani. Na akawapandisha wazazi wake kwenye kiti cha enzi. Na wote wakaporomoka kumsujudia."*(99,100). Aya za mwisho zinasisitiza mafunzo ya hicho kisa chenyewe: *"Kwa hakika katika hadithi zao* (yaani: za mitume - rhs) *limo zingatio kwa wenye akili. Si maneno yaliyo zuliwa, bali ni ya kusadikisha yaliyo kabla yake, na ufafanuzi wa kila kitu, na ni uwongofu na rehema kwa kaumu yenye kuamini".*

**Matatu ya Thamani**

Kitabu cha Matatu ya Thamani ni mfano wa kwanza kwa maudhui ya 'Yusuf' katika fasihi ya Kiswahili. Kitabu hicho kimetolewa 1975 na kuandikwa na Salim Ali Kibao ambaye ni mjukuu wake Hemed bin Abdallah el-Buhry (1850-1928) aliyekuwa akiitwa Mzee Kibao na kutunga tenzi nyingi mmojawapo maarufu 'Utenzi wa Vita vya Wadachi Kutamalaki Mrima' (Mulokozi na Sengo 1995). Salim Ali Kibao alitunga tungo nyengine, utenzi wake mmoja unaojulikana sana na kupata zawadi ni 'Utenzi wa Uhuru wa Kenya'.

Sijui nikiite kitabu cha Salim Ali Kibao riwaya fupi ama hadithi refu ama kisa kirefu kwani hadi sasa hizo aina za fasihi maandishi na fasihi simulizi pia za Kiswahili hazijaainishwa za kuridhisha (taz. Rollins 1983). Bertoncini (1989:206) amekiita 'novelette', naye Ohly (1990:18) ameandika ni 'short novel'. Kina kurasa 59. Hadithi imegawika katika milango kumi.

Katika milango mine ya mwanzo utoto wa Sudi, kitinda mimba wa Bw Hogo na Bi Pendo umeelezwa. Ndio kwanza tu Sudi anapokwenda shule mama yake akafa na ikambidi Bw Hogo amwoe mwengine. Ndugu zake wakaanza kumchukia kwa vile anavyopendwa na babake. Wakahamia mjini kutafuta kazi. Mara tu Bw Hogo akafariki na baada ya matanga nduguze Sudi wakamnyang'anya pesa zote walioachiwa na baba yao. Mzee mmoja akatokea na kuwaambia si vizuri kumnyima mdogo wao, basi wakampa kidogo tu, yaani shilingi mia tatu, na kurudi mjini.

Sudi aliondoka kwake kutafuta maisha katika nchi ya mbali. Mkahawani akakutana na jambazi aliyemwuzia maneno matatu ambayo ni makubwa sana. Akanunua maneno matatu yafuatayo:

Ukitumwa Tumika,
Ukiaminiwa Jiaminishe,
Ukiona la Ajabu Liangalie.

Kwa kutumia neno la kwanza anafuzu kupata kazi nzuri nyumbani kwa Mfalme wa nchi aliyofika. Mfalme, jina lake Ununu, akamwamini Sudi na kumpenda sana, ingawa mawaziri wanajaribu kila njia kumfitini kwa Mfalme, lakini hawasikilizi kwa jinsi anavyompenda. Ikawa:

> Malkia alikuwa kadiri ya makamo ya mama yake hasa, na alimheshimu sana, hata ilikuwa haimjii fikra ya kumtamani hata kidogo. Iliyokuwapo ni heshima tu, kumbe sivyo. Malkia hana umama wala uwana. Mawazo yamemharibikia kabisa hata haoni haya bali atimize tu atakavyo. Sudi alipofika, Malkia hakusita; alianza kumweleza haja yake moja kwa moja kwa kumfanyia ishara za kila namna ya vitinvi. (...)
>
> Sudi akamwambia: (...) Basi nami nipe nafasi japo hii leo tu halafu nitakujibu. (...)

> Lakini wapi; usingizi haukuja upesi kwani alifikiri sana usiku ule, likamjia neno la pili alilonunua kwa shilingi mia nalo ni 'UKIAMINIWA JIAMINISHE'. Hapo akajishauri, 'Lau akiniita tena nitamwambia habari hii bila ya kuchelewa na ndilo litakalokuwa jawabu langu zuri sana la kumkatisha tamaa, kwani siwezi kumtimizia haja atakayo kwangu hata kidogo.

Malkia aliudhika sana kwa kukataliwa na Sudi. Akamfitini Sudi kwa mumewe naye Mfalme hakutaka kumuudhi Malkia, kwa hivyo akakubali Sudi auawe. Sudi akatumwa kuipeleka barua kwenye mapango ya vifo ambapo auawe afikapo tu. Lakini njiani akaona mtu mrefu sana, akaona ajabu sana. Akataka aangalie kwa karibu zaidi, hasa anapokumbuka neno la tatu. Alichelewa sana na kukutana njiani na wafanya kazi wa mapango ya vifo wakiwa wanarudi kutoka kazini kwao. Akawapa barua na kurudi nyumbani kwa mfalme. Lakini wakati huo huo Malkia akawa hakuweza kujizuia kwa vile alivyojaa kisasi na kutaka kumwona Sudi kuuawa. Akawa alijifungafunga mashuka ili asijulikane, basi akafika kwenye mapango kabla Sudi hajafika. Kuingia tu akauawa badala ya Sudi. Baada ya kugundua kifo cha mkewe Mfalme akaelezwa na Sudi yote yaliyotokea: yeye Sudi alivyodhulumiwa na kaka zake, alivyouziwa maneno matatu na vipi hayo maneno yalivyomfikisha alipo sasa.

Katika milango miwili ya mwisho Mfalme ambaye alikuwa hana mtoto akampa Sudi ufalme na mwenyewe Mzee Ununu akawa ni mshauri wake. Kisha Mzee Ununu akafariki, naye Sudi akaoa. Muda wote huo kaka zake waliishiwa kabisa na pesa. Walipotafuta msaada wakafikishwa mbele ya Mfalme, ndiye Sudi mdogo wao:

> Hawakumtambua hata kidogo, lakini Sudi alipowaona tu, aliwatambua kuwa ni kaka zake.

Sudi akawahoji juu ya yote yaliyopita na mwishowe wakamweleza ukweli:

> Baba yetu alikuwa tajiri. Alipofariki, tukagawana mali sote watatu, lakini huyu mdogo tukamwona ni mdogo sana hivyo tulimpunja tukampa kidogo sana.

Basi Sudi alijijulisha na kuwasamehe kaka zake baada ya kuombewa radhi nao. Alipowaangalia nduguze akasema moyoni mwake:

> Mlinidhulumu mkanifukuza, lakini Mungu hakunitupa, ameniweka na kunitukuza mpaka hapa nilipofika na ninyi mmekuja wenyewe kuniangukia na kutaka msaada kwangu. Mimi sina nia mbaya kwa mtu yeyote yule anijae kwa haja, sembuse ninyi kaka zangu? (...)

Ikawa:

> Baada ya kuishi kwa muda, aliwatafutia wake, wakaoa: nao wakawa na jamii zao, wakakaa raha mustarehe.

**Maneno Matatu (kwa Reale Elfu Tatu)**

Bertoncini (1989:284) ameandika kuwa hadithi hiyo ya 'Matatu ya Thamani' ni "a traditional tale retold by a modern writer", yaani ni hadithi ya mapokeo ambayo yamesimuliwa upya na mwandishi wa kisasa. Nadhani ni kweli, ingawa sifikiri ni hadithi moja tu ambayo imesimuliwa tena bali ni muungano wa hadithi mbili au huenda hadithi tatu. Mtindo wa lugha iliyomo

kitabuni humo ni zaidi masimulizi kuliko maandishi, si kwa sababu yamo mazungumzo moja kwa moja tu, bali kwa vile mwandishi anavyosimulia, kutomaliza sentensi zake, kubadilisha kiima kati kati ya sentensi na maneno aliyoamua kuyatumia. Zaidi unamsikia mtu anavyokusimulia hadithi hii kuliko kusoma aliyoandika yule mwandishi. Kwa nini ni 'hadithi ya mapokeo'?

Katika kitabu chake chenye mkusanyiko wa fasihi ya Kiswahili, *Anthologie aus der Suaheli-Litteratur* (1894), Carl Gotthilf Büttner alichapisha katika sehemu ya 'Hekaya na Visa' hadithi mbili ambazo moja inaitwa 'Maneno Matatu' na nyengine 'Maneno matatu kwa reale elfu tatu'. Hizo hadithi mbili ambazo zinatafautiana kidogo tu, Büttner alikuwa ameandikiwa na Amur bin Nasur il-Omeiri. Bw Amur Nasur alikuwa ni mwalimu katika Chuo cha Lugha za Kimashiriki cha Berlin. Mwisho wa mojawapo ya hadithi hizo mbili aliandika:

> Na mimi nimeipata kwa ndugu yangu Khalid bin Muhammed bin Surur il-Omeiri katika Unguja na mimi nataka kuibadili kwa lugha dachi kwa bwana wangu iddaktari Bittner (sic) mwalimu wa lugha ya kiswahili. Wasalam. Tamat bikheiri. (Büttner 1894:102)

Hadithi ya kwanza inaeleza habari ya kijana mmoja ambaye baada ya kufiwa na wazazi wake na kurithi elfu tatu, anahamia mji mwengine. Huko anafunguliwa duka na sheikh tajiri. Hana la kuuza ila maneno matatu tu aliyoachiwa na baba yake kama wasia. Anataka auze kila neno moja reale elfu mbili. Siku moja akapita kijana mgeni dukani kwake. Huyo pia alikuwa amerithi kwa baba yake. Karithi elfu sita ambazo zinamtosha kuyanunua haya maneno matatu yafuatayo:

> Ukiona neno usinene neno na ukinena neno litakujia neno, wasalam
>
> Ukisafiri katika bara jua likikuchwea njiani lala hata na kama unakokwenda unakuona Allah Allah lala, wa salaam
>
> Ukienda njiani ukiona mtu akakukarabisha ya kwanza mwambie astarehe, mara ya pili kazalika, mara ya tatu, tafadhal kaa kitako, wa salaam.

Yule kijana anaendelea na safari yake. Safarini neno la pili alilonunua likamsaidia asiuawe kama alivyouawa mwenzake aliyekuwa akisafari naye, pamoja na ngamia. Njiani akakutana na Sultani ambaye anampa kazi ya kumtilia kahawa. Huyo Sultani anampenda sana na kumwamini hadi akampa cheo nyumbani mwake. Siku moja Sultani akamtuma chumbani kwa mke wake mdogo alikosahau saa yake:

> Akaenda yule kijana hatta akafika akaingia ndani akaingia chumbani akamkuta yule mke wa sultani na waziri katika kitanda cha sultani wamelala. Yule kijana asiseme neno akatazama kazi yake aliyotumwa akafanya akaichukua ile saa akaenda zake akafunga mlango vilevile akaenda hatta akafika kwa sultani akampa saa. Yule sultani akamwambia: nini khabari ya nyumbani. Akamwambia: kheiri.

Yule kijana alikumbuka neno la pili na hakumwambia sultan. Basi huyo waziri alijaa hofu ya kuwa sultani ataambiwa yaliyotokea na yule kijana, akatoa amri shimo lichimbwe huko shamba. Kisha akamtuma yule kijana shamba atiwe shimoni. Lakini kwa kufuata shauri la neno la tatu yule kijana akachelewa kufika shambani penye shimo. Akamkuta waziri aliyekwenda kutazama kama kazi imefanyika, ametiwa ndani mwenyewe na kuuawa.

> Bassi, wakarudi mjini hatta wakenenda kwa sultani, sultani akamwuliza: mnatoka wapi? Yule kijana akasema: tunatoka shamba. Yule kijana akasema khabari ya waziri yote tokea mwanzo hatta mwisho. Na khalafu akasema khabari yake yote alionunulia maneno kwa reale elfu sita. Sultani akamwambia: maneno hayo ulionunua ni ghali. Akampa elfu ishrini na sita akamwambia wewe sasa waziri wangu mkubwa, wa salaam.

Hadithi ya pili (Büttner:125-130)ya Bw Amur Nasur inatafautiana na ya kwanza katika mambo madogomadogo tu: nchi yenyewe ni 'Mekrani', saa ndogo ni saa ya mkono, Sultani ana wake wawili na masuria talatha mia, shimo ni handaki, neno la kwanza ni tafauti kidogo - *"Ukiona neno isinene neno, ukinena neno litakupata neno"*. Lakini mfumo na mtiririko wa hadithi ni ule ule.

Ni wazi kabisa kuwa Salim Ali Kibao ana vipengee vingi katika *Matatu ya Thamani* yake vinavyolingana na hadithi hizo mbili katika kitabu cha Büttner, lakini mtiririko muhimu sana katika kitabu chake, yaani Sudi kutupwa na kaka zake na mwishowe kuwaona tena akiwa mfalme yeye, unakoseka katika 'Maneno Matatu' na 'Maneno Matatu kwa Reale Elfu Tatu'. Maudhui ya riwaya ya Salim Ali Kibao ni sawa na Kisa cha Yusuf, na mtiririko wa matukio pia: Sudi kama Saidna Yusuf anadhulumiwa na kaka zake kwa sababu ya kijicho walicho nacho, na baba yao anavyompendelea. Naye Sudi pia hampiti kinyume mfadhili wake kwa uaminifu wake. Mwishoni akatunukiwa kwa kupewa ufalme na hao waliomtesa tena kaka zake wakaja kumwangukia na kuomba radhi.

Sehemu moja ya hadithi za Amur Nasur inatia wasiwasi kidogo. Yule kijana pia anapendwa na kuaminiwa sana na mfalme aliyempatia nafasi katika nyumba yake, tena nafasi ya uaminifu kwa kiasi anavyoweza hata kuingia chumbani kwa mkewe mfalme. Lakini hapa si kijana anayetamaniwa mwenyewe na hatari ya kuvunja uaminifu wake, bali ni waziri na mke mdogo wa mfalme wanafumaniwa naye. Nalo neno alilonunua linamsaidia asimwambie mfalme ingawa baada ya kuuawa kwa waziri anamwambia mfalme yote yaliyotokea. Ijapokuwa sehemu hii inatafautiana na 'Matatu ya Thamani' na 'Kisa cha Yusuf' na tukio lenyewe ni tafauti, mada ni ile ile yaani Yusuf inambidi athibitishe uaminifu wake. Hata mtu angeweza kufikiri kwamba hiyo sehemu pia inahusiana na Kisa cha Yusuf.

Uhusiano baina ya 'Matatu ya Thamani' na 'Kisa cha Yusuf' hauonekani katika maudhui tu, bali neno la kwanza la 'Ukitumwa Tumika' linatusaidia kupata asili yake. Maana, je uhusiano huu ni moja kwa moja baina ya kitabu cha Salim Ali Kibao na Qurani, ama tutafute kwengine? Kwa hakika neno hilo la kwanza tunalikuta katika maandishi mengine ya fasihi ya Kiswahili ingawa kidogo tu tofauti na katika lahaja tofauti, lakini kwenye muktadha ule ule na lenye maana ile ile.

### Hadithi ya Ya'aqubu na Yusufu

Katika ubeti wa 237 wa utendi wa Ya'aqubu na Yusuf, Yusuf anamwambia Zulekha mkewe 'Azizi:

> Ni mtumwa kwa hakika   nituma nitatumika,
> kupeya maji kuteka   tayari ukinambia.

Utendi huu umetungwa kwa lahaja ya kaskazini. Kipande cha pili cha mshororo wa kwanza kina ujumbe ule ule neno la kwanza la Matatu ya Thamani lililo nao: 'nituma' kwa lahaja za kaskazini ni sawa sawa na 'nitume' kwa lahaja za kusini. Yusuf anamwambia Zulekha (au watu wengine husema Zalikha): 'nitume nitatumika'; Sudi anaambiwa na neno lake la kwanza: 'ukitumwa tumika'.

Utendi huu umehaririwa na Knappert katika *Four Swahili Epics* kwa harufi za Kirumi mwaka 1964 na kutolewa Leiden, Uholanzi, bila mtoaji kutajwa. Miaka 21 baadaye yeye Knappert amechapisha tafsiri yake kwa Kiingereza katika *Islamic Legends* (1985). Mara nyingi tafsiri hii siyo tafsiri ya maneno yote ya utenzi huo bali ni ufupisho au mukhtasari beti kadhaa pamoja.

Katika utangulizi wa *Four Swahili Epics* anaeleza kuwa Utenzi wa Yusuf umetajwa na Alice Werner kwa mara ya kwanza mwaka 1918, lakini hati zake zimepotea na haijulikani kama utenzi aliouchapisha Knappert ni ule aliotaja Bi Werner. Katalogi ya *"Hati na Kanda za Kiswahili na Kiarabu katika Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam "*(Allen:1970) inataja hati sita ambazo zimo makatabani humo. Knappert alitumia hati tatu kwa toleo lake la utenzi huu, lakini hakutia aya za Qurani ambazo zimo katika hati zote kati kati ya beti za utenzi. Mara nyengine anabadilisha lahaja iliyotumika, kwa mfano 'kwanda' iwe 'kwanza', na kadhalika.

Hati ambayo nimeiona na kupata nakala yake imo maktaba ya Chuo Kikuu cha Hamburg. Imeandikwa na Mohamed Kijumwa mwezi 20 Muharram 1332, yaani mwaka 1913. Naye Dammann anaeleza katika katalogi yake (Dammann 1993:35) kuwa Mohamed Kijumwa aliandika nakala nyengine yenye jina 'Qissat-ilYusuf' aliyompelekea mwaka 1937. Naye Knappert anafikiri pengine ndiye Muhammad b. Abu Bakari Kijuma wa Lamu aliyetunga utenzi huu.

Utenzi huo una beti 737. Unaeleza kwa urefu hadithi ilivyo katika Qurani, lakini unaeleza zaidi, maana muna mengi ambayo hamna katika Qurani. Kwanza mna wahusika wengi ambao majina yao hayakutajwa katika Qurani: Zulekha, malkia na mkewe 'Azizi ambaye humu si waziri bali ni mfalme wa Misri; Katufiri (Potafia katika Biblia) aliyemnunua Yusuf kisha kampa mfalme 'Azizi; Bunyamini, mdogo wake Yusuf wa mama mmoja; Jiburili, jini mwema mwanamke isilama, anayemkinga Yusuf; Yahudha, kaka yake, kifungua mimba; Maliku bin Dhahari, mkuu wa msafara aliyemnunua Yusuf na kumwuza huko Misri; Barilii, mwanawe mfalme ambaye alikuwa ameolewa na Katufiri na baada ya kifo chake kuolewa na Yusuf; Rahili, mama yao Yusuf na Bunyamini; Furathima na Misha na Rehema, wote watatu wanawe Yusuf na Zulekha ambao mwishowe wanaoana.

Inavyoonekana kutokana na majina hayo yote, hadithi hii ina matukio mengi pia ambayo hatuyajui kutokana na Qurani. Mengine yanajulikana kutokana na Biblia na kutafautiana nayo kidogo, mengine yanajulikana katika ushairi wa nchi kama vile Uajemi na Indonesia. Kwa jumla kiini cha habari, mtiririko wa kisa na maudhui yake ni sawa sawa:

Zulekha akimuona     kadangana katatana
kampenda mno sana     mahaba yakamngiya

Mahaba yakamshika asiweze kamtaka
Yusufu akatamka mimi Mungu hujichea

Mumeo amekwetea mimi kukutumikia
kwa upendalo nambia tatumika mara mia

Mumeo ndiye bwanangu na fadhili nyingi kwangu
ni muhali hilo kwangu mimi sitokuridhia

Nana wewe hufahamu hanali kulla dhalimu
na mimi ni Isilamu yote hayo hunelea (Knappert 1964:25, 230-234)

Hata hivyo mtungaji alipokuwa akipanua habari yenyewe kusisitiza kipengee fulani, kutia chumvi au kinyume chake kupunguza umuhimu wa kitu fulani, maudhui hayakubadilisha, kwa mfano:

Mak'etiyo yalo kweli mwanamke na rijali
ikakoma hiyo hali ya Yusufu nakwambiya

Mahaba yakamngia ili kumuinukia
kasahau yote pia katikati kamngia

Akamuona babake akafunga moyo wake
yale mahaba yake yote yakampotea (beti 253-255)

Jiburili akafuza chanda chake kamwekeza
tena kumsimangiza Yusufu huwata ndiya

Na diwani ya Mitumi wandishiwe si usemi
nimezoona ni mimi utafutwa nakwambiya

Yusufu akisikiya mbiyo akaiyondokeya
Zulekha akamtupiya bwana ninni nambiya (beti 259-261)

Ndio ubwingwa wa mtungaji unaotupa picha vipi Yusuf alifaulu kukinga uaminifu wake. Hapa si lugha yenyewe iliyo na nguvu fulani, pia arudhi ya hii fani ya utenzi, yaani kuimba kwake, pamoja na vina na mizani, tena hayo yote yanamsaidia msikilizaji ahifadhi hadithi yenyewe kwa urahisi zaidi. Kwani tenzi zenyewe kimsingi zilikuwa ni fasihi simulizi.

**Paradise**

Mfano wa mwisho wa maudhui ya 'Yusuf' katika fasihi ya Kiswahili ni kitabu cha Kiswahili kwa Kiingereza, yaani karibu yote yaliyomo ni mambo ya Kiswahili, ustaarabu na utamaduni wake, maisha, watu wanavyozumgumza, wanavyotenda, mahali wanapofika na vitendo vinapotendeka. Hata maneno mengi ya Kiswahili yamo bila tafsiri yoyote, ijapokuwa kitabu chote kimeandikwa kwa Kiingereza. Magazeti yote yalikubaliana kwa kusema ni kitabu cha hali ya juu na mtu anaweza akakilinganisha na vitabu vya Conrad. Jina lake *Paradise* na mwandishi wake Abdulrazak Gurnah ambaye kazaliwa Zanzibar. Sasa hivi anafundisha fasihi

Chuo Kikuu cha Kent, Uingereza. Kitabu kimetolewa 1994 na kutajwa rasmi kwa zawadi ya 1994 Booker Prize. Kwa bahati mbaya hakikupata hiyo zawadi.

Mhusika mkuu wa riwaya hii ni kijana Yusuf. Nao Zulekha na Azizi wamo, tena kwa majina yale yale. Yusuf amepelekwa kwa tajiri Aziz ambaye ni mfanya biashara mkubwa mwanzoni mwa karne hii wakati Wajerumani walipokuwepo Tanganyika. Babaake Yusuf anampa Azizi Yusuf kwa sababu ana madeni kwake ambayo anashindwa kulipa. Kitabuni humo Yusuf hauzwi, lakini ni rehani kwa madeni hayo maana hana la kusema. Naye Yusuf kwanza anafanyishwa kazi katika duka dogo huko, halafu dukani kwenye mahala pengine, kisha anachukuliwa safarini pamoja na tajiri wake na msafara mzima. Anaporudi dukani alipoanza kazi yake, Zulekha mkewe Azizi, anayekaa nyumbani nyuma ya duka, anamtaka:

> The room was fragant with incense and the Mistress was sitting alone waiting for him. He stopped at the door, afraid to enter. She smiled and beckoned him in. He saw that she was richly dressed, her long cream dress glittering with amber thread. She pulled her shawl away and leaned forward, waving him nearer with insistent urgency. He took two steps forward and stopped, his heart pounding, knowing he should leave. She began to talk quietly to him. Her voice was rich with feeling, and her smile grew softer as she spoke. Yusuf could not be sure what she wanted him to do, but he could not mistake the look of passion and longing on her face. She pressed the palms of her hand on her bosom and rose to her feet. When she put her hand on his shoulder he shivered. He began to retreat and she followed. He turned to flee, but she clutched his shirt from behind and he felt it tear in her hands. As he ran out of the room, he heard her screams of agony but did not look back or hesitate. (Gurnah 1995:236)

Mtiririko si sawa na ule wa Kisa cha Yusuf, lakini wahusika wakuu wamo, taswira imo na maudhui yenyewe yamo. Mwisho tu wa kitabu unatafautiana sana na hatima ya Kisa cha Yusuf, yaani Yusuf hapati cheo kikubwa wala kuungana tena na watu wa asili yake. Yusuf wa Gurnah hata hatujui ataamua kufanya nini, pengine atafuatana na askari wa Kijerumani, pengine atabaki alipo.

**Mwisho**

Katika makala haya nimejaribu kuonyesha maudhui ya Yusuf yametekelezwa vipi katika fani chache za Kiswahili. Nimeanza na tafsir za Qurani nikafikia *Paradise* ya Abdulrazak Gurnah. Hata ziko zaidi ambazo sijazipitia, k.m. utenzi wa Yusuf wa Said Karama (1964) au tenzi nyengine ziuzwazo kwenye kaseti huko Afrika Mashariki. Kulinganisha kwenyewe kuna hatari yake na faida yake, kwani tunalinganisha nini?

Maudhui ya Yusuf yapatikana katika fasihi ya dunia: kuanzia hekaya za Kimisri miaka 1500 kabla ya Kristo; kuendelea na habari ya Yusuf katika *Biblia* kwa Mayahudi; kupitia tanzia ('tragedy') ya *Hippolytos* ya Euripides kwa Wagiriki na tamthiliya ya *Phaedra* ya Seneca kwa Warumi; kupitia tungo za Firdausi huko Uajemi, mpaka *Joseph and Seine Brüder* ya Thomas Mann hapo Ujerumani na kufikia *Paradise* ya Abdulrazak Gurnah.

Kwa hakika elimu ya Fasihi Linganishi (Comparative Literature) ingeweza kuanzisha elimu peke yake ya "Yusuf", tuseme "Yusufikia".

Lakini maudhui yenyewe yanaanzia wapi na kuishia wapi? Maudhui yenyewe ni ya kilimwengu:

- mapenzi - baba anavyompendelea mwanawe mmoja;
- wivu - ndugu wanavyomwonea ndugu mmoja kijicho;
- safari katika nchi ya kigeni - Yusuf huko Misri;
- mahaba - Yusuf anatamaniwa na Zuleikha;
- uaminifu na tunzo yake - Yusuf anapewa cheo;
- rehema - Yusuf anawasamehe nduguze.

Turudi kwenye mifano yetu kutoka fasihi ya Kiswahili. Katika uchambuzi wa fasihi ya Kiswahili mara nyingi watu hujaribu kuchambua nini kienyeji , nini kigeni, kipengele gani cha Kiafrika, kipi cha Kiarabu au tuseme Kimashiriki.

Nimejaribu kuonyesha vipi hadithi ya Mzee Kibao ilivyoathiriwa na kisa cha Yusuf pamoja na hadithi za Amur Nasur; nimeshindwa kuamua kuwa hadithi za Amur Nasur zimeathiriwa na kisa cha Yusuf au la, yaani humo yule kijana kweli ni Yusuf naye mke wa mfalme ndiye Zuleikha, au hata waziri mwenyewe amechukua nafasi ya Zuleikha?

*Utenzi wa Yaaqubu na Yusuf* una mengi unayokuta katika utungo mrefu (maana ni kitabu kizima) wa Mwajemi, jina lake Abd al-Rahman Jami, aliyeutunga mwaka 1484. Hata Sh Yusuf Ali anautaja utungo huo katika tafsir yake ya Quran (1938, 1977). Utungo huo wa Jami umeathiri tungo nyingi za kisa cha Yusuf katika lugha kadhawakadha, k.v. kwa Kiurdu na Kijava na tungo nyingi za Kipanjabi (Shackle 1995).

Lakini muna mengine katika *Utenzi wa Yaaqubu na Yusuf* ambayo hatuyakuti katika msahafu wala katika utungo huo wa Jami. Maadam jamii fulani imefanya dhana au maudhui yenyewe iwe sehemu ya jamii hiyo, iwe mada muhimu ya ustaarabu na utamaduni wake, kwa hivyo: hamna 'kigeni' tena.

Ni sawa sawa na maana ya maneno yenye asili ya Kiarabu kwa Kiswahili. Katika kulinganisha Surat-il-Yusuf na tafsir zake nimeona mifano mingi ya aina hiyo ya mabadiliko ya maana:

كَيْدٌ [kaid] za kaka zake Yusuf na za Zuleikha si „kedi" kwa Kiswahili, ingawa Kiswahili kina „kedi" pia, bali imetafsiriwa na „hila" au „vitimbi" au „zitimbi", ijapokuwa Kiarabu kina „hila" vile vile;

قِصَّةٌ [qissa] imetafsiriwa kwa Kiswahili „simulizi" na „kisa" pia; na imetafsiriwa „hadithi", „visa" na „mafumbo";

تَفْسِيرٌ [tafsiir] si „tafsiri" au „-tafisiri" ya Kiswahili, na kwa maana yake ya Kiarabu Sh Ali Muhsin hutumia „tarjama" au „-tarjimu", maanake „to translate";

فِتْنَةٌ [fitna] ya Kiarabu si ile „fitna" au „fitina" tunayoijua kwa Kiswahili.

Nini 'kigeni', nini 'kienyeji?

Nitapenda nimalize pale nilipoanza. Wafulbe huandikiwa kombe „HAMMATBIHI WAHAMMABIHA" na nisingeshangaa Waswahili wengine wafanye vivyo hivyo. Wamechukua dhana hiyo, wazo hilo, na kulifanye liwe sehemu ya maisha yao, mila na desturi yao, utamaduni wao, fasihi yao. Wafasiri wametafsiri maneno hayo kwa Kiswahili:

(.....) alimtamani (.....) na angeli mtamani.

Kwa nini kwa Kiswahili mara kuna tafauti katika alama za wakati? Basi, tuitazame hiyo sehemu kamili ya Qurani na tafsiri yake kwa Kiswahili:

وَلَقَدْ هَمَّتْ بِهِۦ وَهَمَّ بِهَا لَوْلَآ أَن رَّءَا بُرْهَٰنَ رَبِّهِۦ ۚ كَذَٰلِكَ لِنَصْرِفَ
عَنْهُ ٱلسُّوٓءَ وَٱلْفَحْشَآءَ ۚ إِنَّهُۥ مِنْ عِبَادِنَا ٱلْمُخْلَصِينَ

(12:24) "*Na hakika yule mwanamke alimtamani, na Yusuf angeli mtamani lau kuwa hakuona ishara ya Mola wake Mlezi. Hayo hivyo ni kwa ajili tumuepushe na uovu na uchafu. Hakika yeye alikuwa katika waja wetu walio safishwa.*"

**Marejeo**

Abdulrazak Gurnah. 1995. *Paradise*. London: Penguin.

'Abdullah Yusuf Ali. 1991. *The Meaning of the Holy Quran*. Maryland: Amana Corporation.

Allen, J.W.T. 1970. *Catalogue of Manuscripts and Tapes in Arabic and Swahili in the Library of the University College of Dar es Salaam*. Leiden: Brill.

Bertoncini, Elena. 1989. *Outline of Swahili Literature: Prose Fiction and Drama*. Leiden: Brill.

Büttner, Dr. C. G. 1894. *Anthologie aus der Suaheli-Litteratur*. Berlin: Emil Felber. K. 97 - 102 na 125 - 130.

Dale, Godfrey. 1923. *Tafsiri ya Kurani ya Kiarabu*. London: Society for Promoting Christian Knowledge.

Dammann, Ernst. 1993. *Afrikanische Handschriften. Teil 1*. Stuttgart: Franz Steiner.

Knappert, Dr. J. 1964. *Four Swahili Epics*. Leiden. p. 5-58.

Knappert, Jan. 1985. *Islamic Legends*. Leiden: Brill. p. 85-104.

Mulokozi, M. M. and T.S.Y. Sengo. 1995. *History of Kiswahili Poetry [AD 1000 - 2000]* Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.

Ohly, Rajmund. 1990. *The Zanzibar Challenge*. Windhoek: University of Namibia.

Rollins, Jack D. 1983. *A History of Swahili Prose*. Leiden: Brill.

Said Karama. 1968. *Utenzi wa Nabii Yusuf.* Mombasa: Haji Mohamed & Sons.

Salim A. Kibao. 1975. *Matatu ya Thamani.* Nairobi: Heinemann Educational Books.

Shackle, Christopher. 1995. "Between Scripture and Romance: The Yusuf-Zulaikha Story in Panjabi." *South Asia Research* 15,2.

Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy. 1984 (1969). *Qurani Takatifu.* Nairobi: The Islamic Foundation.

Sheikh Ali Muhsin Al-Barwani. 1995. *Tarjama ya "AL MUNTAKHAB" Katika Tafsiri ya QUR'ANI TUKUFU.* Abu Dhabi: Taasisi ya Zayed bin Sultan Al-Nahayan.

Sheikh Mubarak Ahmad Ahmadi H.A. 1953. *Kurani Tukufu.* Nairobi, Tabora: E. A. Ahmadiyya Muslim Mission.

Yohannan, John D. (edited with commentary) 1968. *Joseph and Potiphar's Wife in World Literature.* New York: New Directions Publ.